**HOTUBA YA RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI MHESHIMIWA DK. HUSSEIN ALI MWINYI KATIKA UFUNGUZI WA JENGO LA HUDUMA ZA MATIBABU YA DHARURA NA MAABARA KWENYE KITUO CHA AFYA MAKUNDUCHI WILAYA YA KUSINI MKOA WA KUSINI - UNGUJA**

**17 JANUARI 2024**

**Waheshimiwa mawaziri Mliopo**

**Mheshimiwa Hassan Khamis Hafidh, Naibu Waziri wa Afya Zanzibar,**

**Mheshimiwa Ayoub, Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja,**

**Mhandisi Zena Ahmed Said, Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi,**

**Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Kusini Unguja,**

**Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Kusini Unguja,**

**Dkt Amour Suleiman Mohamed, Kaimu Katibu Mkuu na Mkurugenzi Mkuu Wizara ya Afya**

**Viongozi wa vikosi vya ulinzi na Usalama mliopo,**

**Waheshimiwa Wabunge na Wawakilishi mliopo**

**Wakurugenzi wa Wizara ya Afya na Wizara nyengine mliopo,**

**Mwenyekiti wa CCM, Wilaya ya Kusini,**

**Viongozi wa Vyama na Serikali mliopo,**

**Ndugu wafanyakazi na waandishi wa habari**

**Wageni waalikwa,**

**Ndugu Wananchi,**

**Mabibi na Mabwana,**

**ASSALAM ALAYKUM**

Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na afya njema na kutuwezesha kukutana kwa madhumuni ya kulifungua rasmi jengo jipya la Huduma za matibabu ya dharura na Maabara ya kisasa katika kituo chetu cha Afya hapa Makunduchi. Napata faraja kuhudhuria tukio hili kwani wiki chache zilizopita, nilipokuja Makunduchi kwa ajili ya kisomo cha Duwa, niliwaahidi viongozi wakiwemo masheha kuwa penye majaaliwa, nitakuja mwenyewe katika sherehe za ufunguzi wa jengo hili. Namshukuru Mwenyezi Mungu kuniwezesha kufikia dhamira yangu hiyo. Aidha, naishukuru Wizara ya Afya na wafadhili waliondaa shughuli hii ya leo na kwa heshima waliyonipa ya kuwa Mgeni Rasmi. Pia, natoa shukrani zangu za dhati kwenu ndugu wananchi, viongozi na waalikwa wote kwa kuamua kuja kuungana nasi katika tukio hili muhimu la maendeleo ya sekta ya afya.

**Ndugu Wananchi**,

Ujenzi wa jengo jipya la huduma za matibabu ya dharura na maabara ya kisasa hapa Makunduchi ni miongoni mwa juhudi zinazochukuliwa na Serikali katika kuimarisha miundombinu ya huduma za Afya ili ziweze kwenda sambamba na mabadiliko ya maendeleo ya huduma za afya duniani. Hatua hii vile vile ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020- 2025 pamoja na ahadi tulizozitoa wakati wa kampeni

za uchaguzi mkuu mwaka 2020. Nyote ni mashahidi wa mafanikio ambayo tumeyapata katika kipindi cha miaka mitatu tu ya uongozi wa Awamu ya Nane katika kuimarisha sekta ya afya kama ilivyo katika sekta nyengine zikiwemo elimu, maji safi na salama, umeme, ujenzi wa barabara na nyenginezo.

Katika sekta hii ya afya, tunathibitisha utekelezaji wa ahadi zetu kwa kumaliza kujenga na kufungua hospitali 10 za wilaya na moja ya mkoa ya Lumumba ambazo zote tumeziwekea vifaa vya kisasa na wataalamu kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi kwa mujibu wa ngazi ya hospitali husika. Leo hii tupo hapa Makunduchi katika tukio jengine la ufunguzi rasmi wa jengo jipya la huduma za tiba za dharura pamoja na maabara ya kisasa. Huu ni mwendelezo wa mageuzi makubwa ya maendeleo ya sekta ya afya hapa nchini.

**Ndugu wananchi,**

Serikali ya Awamu ya Nane inaendelea kuchukua hatua mbali mbali za kuimarisha huduma za afya katika ngazi zote. Tumekamilisha ujenzi wa Hospitali katika ngazi ya wilaya na kuanza ngazi ya mkoa. Tutaendelea kujenga hospitali za mikoa katika mikoa iliyobaki ikiwemo Mkoa huu wa Kusini Unguja ambapo taarifa njema ni kuwa mfadhili ameshapatikana. Eneo lipo tayari na mfadhili ameshawasilisha michoro ya awali ya hospitali hiyo itakavyokuwa. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali pia inaendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma za Afya kwa ngazi ya msingi. Hatua hiyo ni utekelezaji wa mpango mpya wa serikali katika utoaji wa huduma za Afya

ngazi ya msingi ikiwa ni pamoja na kuimarisha miundombinu kwa kujenga majengo mapya na kutanua baadhi ya vituo vya afya nchi nzima, kuweka vifaa vya kisasa kwa lengo la kutoa huduma bora za afya ikiwemo za dharura na uchunguzi wa awali katika ngazi ya msingi ili kupunguza vifo visivyotarajiwa.

**Ndugu wananchi,**

Serikali imepata mafanikio makubwa katika utekelezaji wa mipango na mikakati ya kuendeleza sekta ya afya nchini kupitia programu mbali mbali zinazoendeshwa kwa ushirikiano na Washirika wa Maendeleo. Jambo hilo limesaidia kuimarisha huduma za afya katika ngazi ya msingi. Vile vile ujenzi wa miundombinu kama hii na utoaji wa elimu ya afya na uibuaji wa wananchi wenye matatizo mbali mbali ya kiafya mapema kupitia programu hizi ikiwemo ya wafanyakazi wetu katika ngazi ya jamii (CHW) tuliyoizindua rasmi tarehe 16 Disemba 2023 pale Maisara mjini Zanzibar na Afya Call Center. Huduma ambayo mwananchi sasa anaweza kupiga simu kupitia namba 190 bure na kupata ushauri wa kiafya. Serikali ina lengo la kuunganisha kituo hiki muhimu na huduma za dharura nchi nzima. Jambo hili linaisaidia serikali kuimarisha afya ya jamii, mfumo wa rufaa, kupunguza vifo pamoja na kupunguza gharama za matibabu kwani wagonjwa hupatiwa matibabu mapema na kupewa ushauri unaofaa ili kupambana na magonjwa yasiyoambukiza ikiwemo kisukari, presha na saratani.

**Ndugu wananchi,**

Serikali ya awamu ya nane imelenga kuzisogeza huduma zote muhimu za afya kuwa karibu zaidi na wananchi ikiwa ni pamoja na kuweka mifumo ya TEHAMA na upatikanaji wa dawa na vifaa tiba muhimu ili kurahisisha upatikanaji wa huduma za matibabu na uchunguzi kwa wananchi wote kwa wakati na bila ya usumbufu wowote. Nitumie nafasi hii kuitaka Wizara ya Afya kwa kushirikiana na wafadhili wetu, kuhakikisha kituo hiki kinakuwa na wafanyakazi wenye sifa na uwezo unaohitajika na kinawekewa mifumo na vifaa vya TEHAMA ili kifanye kazi kwa ufanisi zaidi katika kuwahudumia wananchi, pamoja na kuhakikisha mazingira bora ya kazi kwa wahudumu wa afya.

**Ndugu wananchi,**

Nachukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Shirika lisilokuwa la Kiserikali la Uingereza-Health Improvement Project In Zanzibar (HIPZ), kwa kuunga mkono jitihada za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuiimarisha miundombinu ya huduma za afya hapa Zanzibar hasa katika Kituo cha Afya Makunduchi na hospitali ya Kivunge Wilaya ya Kaskazini A. Natoa shukurani zangu kwa kuweza kufanikisha ujenzi wa jengo hili, uwekaji wa vifaa tiba vya kisasa kabisa pamoja kuwajengea uwezo wafanyakazi wetu ili waweze kutoa huduma zilizo bora kulingana na miongozo iliyowekwa. Natoa shukurani wa washirika wetu wote wa maendeleo wanaoshirikiana na Serikali katika kufanikisha dhamira yetu ya kuimarisha huduma za afya hapa Zanzibar.

**Ndugu wananchi,**

Kabla sijamaliza hotuba yangu, nitoe wito kwa wananchi wote kuendelea kuvitumia vituo vyetu vya afya kwani Serikali inaendelea na utekelezaji wa mikakati ya kuimarisha huduma za afya katika ngazi ya msingi kwa kiwango cha hali ya juu. Pale panapohitajika matibabu ya ziada ambayo yanakosekana katika vituo vyetu, basi wataalamu watatushauri kwenda kupata matibabu hayo katika hospitali za Wilaya. Kwasababu tayari kuna hospitali zinaendelea kutoa huduma za ngazi ya wilaya ambayo kwa Wilaya hii ya Kusini tunayo pale Kitogani.

Nimalizie kwa kutoa shukurani zangu tena kwa Wizara ya Afya na Wafadhili wetu kwa kukamilisha ujenzi wa jengo hili la kisasa la maabara pamoja na maandalizi mazuri ya shughuli hii. Nawashukuru watu wote waliofanikisha shughuli hii wakiwemo shehe wetu aliyetusomea Qurani, vijana wetu wa hamasa na watu wote waliofika kuhudhuria tukio hili. Ahadi yangu kwenu ni Serikali yenu kuendelea kutimiza ahadi zake kwenu ambapo najua kazi ya ujenzi wa barabara za ndani inaendelea, ujenzi wa skuli mpya ya ghorofa Makunduchi nao unaendelea na huduma za maji nazo zinaendelea kuimarishwa. Nasaha zangu kwenu muendelee kuiunga mkono Serikali yenu ili tuongeze kasi ya kuwatumikia wananchi na kuwaletea maendeleo zaidi.

Baada ya kusema hayo, naomba sasa nitamke kuwa " **Jengo hili la huduma za matibabu ya dharura na maabara liliopo hapa katika Kituo cha Afya Makunduchi limefunguliwa rasmi**".

**Ahsante sana kwa kunisikiliza**